

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**

Anuani ya Simu: "TAMISEMI"

SimuNa: (026) 2322848, 2321607  
2322853, 2322420

Nukushi: (026) 2322116, 2322146  
2321013

Baruapepe: [ps@tamisemi.go.tz](mailto:ps@tamisemi.go.tz)  
[www.tamisemi.go.tz](http://www.tamisemi.go.tz)



Tawala za Mikoa na  
Serikali za Mitaa,  
Jengo la Mkapa,  
2 Barabara ya Hospitali,  
S.L.P. 1923,  
41185 DODOMA.

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTARATIBU WA UHAMISHO KWA  
WATUMISHI WANAOOMBA KUHAMIA HALMASHAURI ZILIZO NJE YA  
MIKOA YAO**

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) inawajulisha watumishi wote wanaoomba uhamisho kutoka Halmashauri zilizo nje ya Mikoa yao kuwa hawaruhusiwi kufika ofisi za TAMISEMI kuomba uhamisho bali maombi yote yatawasilishwa na Mkoa.

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa inawataka watumishi wote waliomba uhamisho kutoka halmashauri zilizo nje ya Mikoa yao kufuata utaratibu ufutao:

1. Mtumishi anatakiwa kuomba nafasi kwenye Halmashauri anayotaka kuhamia na barua yake ipitishwe na msimamizi wake wa kazi ambaye ni Mkuu wa Idara au Mkuu wa Shule au Mkurugenzi wa Halmashauri.
2. Mtumishi ajibiwe barua na Halmashauri aliyoomba nafasi ikionyesha utayari wa kumpokea na iwapo kuna nafasi.
3. Mtumishi anatakiwa kuandika barua kwa Katibu Tawala wa Mkoa kuomba kibali cha uhamisho kwa kuambatanisha nakala za barua ya kuomba nafasi kwenye Halmashauri anayotaka kuhamia na barua alijojibiwa na Halmashauri aliyoomba nafasi
4. Katibu Tawala wa Mkoa atawasilishwa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa majina ya watumishi wote walokidhi vigezo vya uhamisho na viambatisho vyote vya watumishi walioomba uhamisho
5. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mtaa itatoa kibali cha uhamisho(barua) ambayo itatumika kwa mwajiri wa mtumishi husika na majina kutolewa kwenye Tovuti ya Wizara ([www.tamisemi.go.tz](http://www.tamisemi.go.tz))
6. Watumishi walioomba uhamisho mwaka 2016 na kabla ya uhakiki wa vyeti, ambao vibali vya uhamisho havikutolewa, wawasilishe nakala za barua kwa Katibu Tawala Mkoa zikiwa zimepitishwa na Mkurugenzi wa Halmashauri

Watumishi wanaelekezwa kubaki kwenye vituo vyao vya kazi wakati masuala yao ya uhamisho yanashughulikiwa, Barua za uhamisho zitatumwa kwa waajiri na si vinginevyo.

Imeandaliwa na:

**Rebecca Kwandu**

**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**

**OR - TAMISEMI**

**27 Novemba, 2017**